

BENKI KUU YA TANZANIA
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
TANZANIA

Simu: +255 26 2962586
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz



BANK OF TANZANIA
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
TANZANIA

Phone: +255 26 2962586
Email: botcommunications@bot.go.tz

23 Januari 2022

TAARIFA KWA UMMA

SALAMU ZA RAMBIRAMBI KUFUATIA KIFO CHA GAVANA WA BENKI KUU YA UGANDA, PROF. EMMANUEL TUMUSIIME-MUTEBILE

Benki Kuu ya Tanzania imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Gavana wa Benki Kuu ya Uganda, Prof. Emmanuel Tumusiime-Mutebile, kilichotokea leo asubuhi tarehe 23 Januari 2022 jijini Nairobi, Kenya alikokuwa akitibiwa.

Benki Kuu ya Tanzania inatoa pole kwa Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa Benki Kuu ya Uganda, familia yake, wananchi wa Uganda na jumuiya ya Benki Kuu katika ukanda wetu.

Gavana Tumusiime-Mutebile atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa kwa maendeleo ambayo Benki Kuu ya Uganda imepata katika kipindi cha uongozi wake, ikiwa ni pamoja na kuifanya Benki hiyo kuwa mbele katika matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika utendaji kazi wake, na pia kwa kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha nafasi ya benki kuu katika kufikia mtangamano wa kikanda na ushirikiano wa kiuchumi kupitia Kamati ya Masuala ya Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Akizungumza kufuatia taarifa za kifo hicho, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Prof. Florens Luoga amesema: “Benki Kuu katika kanda yetu zimefaidika sana na mchango mkubwa wa Prof. Tumusiime-Mutebile katika mikutano ya majadiliano ya Kamati ya Masuala ya Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, hasa kutokana na uzoefu wake wa kazi. Tutakumbuka uongozi wake.”

Prof. Tumusiime-Mutebile alianza kuwa Gavana wa Benki Kuu ya Uganda mwaka 2001 hadi mauti ilipomkuta.

Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

BENKI KUU YA TANZANIA